Policy brief TZ.07/2010K

# Wanafunzi wengi zaidi, fedha kidogo

## Matokeo ya Ufuatiliaji wa Matumizi ya fedha za umma (PETS) kwa elimu ya Sekondari





## 1. Utangulizi

Baada ya ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi, Serikali ya Tanzania inatekeleza programu yenye matarajio makubwa ya kupanua elimu ya sekondari. Hata hivyo, upanuzi huu umeleta changamoto nyingine upande wa rasilimali, na kuna maswali mengi juu ya namna sera hii inavyotekelezwa. Je, fedha zinapelekwa kwa utaratibu mzuri? Shule zinapokea fedha kwa wakati? Kiasi kinachofika kinatosha? Muda wa kupata fedha unatabirika? Je, kuna uwajibikaji kwa kushindwa kutekeleza sera? Je, utaratibu mzima wa kutiririsha fedha unahusianaje na ubora wa elimu na utendaji?

Ufuatiliaji wa Matumizi ya fedha za umma ni mojawapo ya zana muhimu za kujibia maswali haya. Mwaka 2009, serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma (*Public Expenditure Tracking Survey*) kwenye elimu ya msingi na sekondari Tanzania bara. Muhtasari huu unawasilisha matokeo muhimu ya ufuatiliaji huu kuhusu namna rasilimali kwa ajili ya elimu ya sekondari zinavyotirishwa, na unachunguza namna ambavyo utaratibu wa kuzifikisha shule unahusiana na ufanisi wa shule. Muhtasari mwingine tofauti umegusia masuala yanayofanana na haya kwa upande wa elimu ya msingi.

Lengo ni kuyafikisha matokeo ya ufuatiliaji kwa hadhira pana, kujenga uelewa kwa jamii kubwa pamoja na kuchagiza mijadala kuhusu mahusiano kati ya matatizo kwenye mtiririko wa rasilimali (*flow of funds*) na ufanisi kwenye elimu. Muhtasari unaonesha kwamba kufumbia macho matatizo haya, kunadhoofisha maendeleo ya elimu na kunaweza kupelekea kukua zaidi kwa tofauti zilizopo katika rasilimali zinazopatikana na ufanisi wa elimu kati ya shule na kati ya Halmashauri.

Uwazi pata picha kamili

Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi iliyopo Twaweza/Hivos Tanzania

Uwazi, S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org

Kimetolewa Septemba 2010

Chanzo cha taarifa zote zilizowasilishwa hapa ni ripoti ya serikali (2010), yenye jina "*Public Expenditure Tracking Survey of primary and secondary Education",* Toleo la Februari 2010, iliyoandaliwa Dar es Salaam, na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.


## 2. Matokeo Muhimu

### Jambo la 1: Fedha zaidi kwa ajili ya elimu, lakini kidogo zaidi kwa elimu ya sekondari

Fungu la bajeti ya elimu linalotengwa kwa ajili ya elimu ya sekondari limekuwa likibadilikabadilika miaka ya hivi karibuni. Likiwa ni asilimia 9.8 mwaka 2008/09, ilikuwa ni kiwango kidogo zaidi kutengewa elimu ya sekondari kwenye bajeti ya elimu katika kipindi cha miaka minne iliyopita. Katika kipindi hiki, uwiano wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa kila mwanafunzi pia ulipungua kwa thamani ya fedha, na kwa kulinganishwa na vitu vinavyoweza kununuliwa na fedha hizo. Katika mwaka wa fedha 2008/09 bajeti iliyotengwa kwa kila mwanafunzi wa elimu ya Sekondari ilikuwa karibu Sh 135,000, ukilinganisha na Sh 281,000 kwa kila mwanafunzi mwaka 2005/06. Katika mwaka wa fedha 2007/08, ambao ufuatiliaji ilichunguza matumizi ya rasilimali za elimu, elimu ya sekondari ilitengewa TSh bilioni 170.2, kiasi ambacho ni sawa na uwiano wa Tsh 150,789 kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa shule.

Hali hii inaibua wasiwasi iwapo kiwango cha rasilimali kinachopangwa kinaendana na dhamira ya Serikali ya kupanua elimu ya sekondari. Kutokana na shule kukabiliwa na hali ngumu, ingetegemewa fedha zaidi zitengwe kwa kila mwanafunzi, na sio kidogo.


**Mchoro1: Mgawo wa bajeti kwa sekta ndogo za elimu 2005/06-2008/09**



## Jambo la 2: Sio fedha zote hutolewa, mapato mengine ya shule lazima yazibe pengo

Kwa mwaka wa fedha 2008, kiasi cha fedha kilichopokewa kwa ajili ya elimu ya sekondari kilikuwa ni asilimia 92 ya bajeti iliyoidhinishwa, kiasi hiki ni kikubwa ukilinganisha na kile cha elimu ya msingi (ambacho kilikuwa ni asilimia 87). Fedha kwa ajili ya kugharimia mishahara na masurufu ya ujira kwa wafanyakazi zilitolewa kama zilivyoidhinishwa. Hata hivyo, haikuwa hivyo kwa upande wa fedha za kununulia vifaa vya kufundishia. Hadi mwishoni wa mwaka wa fedha ni asilimia 56 tu ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia ndio zilikuwa zimetolewa. Ukizingatia umuhimu wa kipengele hiki kwenye kujenga ujuzi, hali hii inaibua maswali ni kwa vipi serikali inawatarajia walimu kufundisha kwa ufanisi na wanafunzi kujifunza vyema wakati vifaa muhimu hawapatiwi?

**Mchoro 2: Maidhinisho ya bajeti, fedha zilizotolewa na matumizi halisi kwenye elimu ya sekondari 2007/08**




Mapungufu haya yanaweza kukuza zaidi tofauti za usawa zilizopo, kwa vile wazazi wanaombwa kuziba pengo lililopo kupitia michango, miradi ya kujitegemea na kutoa chakula.

## Jambo la 3: Fedha zinapelekwa moja kwa moja, lakini hazifiki kwa wakati

Shule za sekondari hupokea fedha kwa ajili ya uendeshaji wake kupitia ofisi ndogo za hazina. Wakuu wa shule wanapoomba fedha, fedha zinatolewa hazina ndogo na kutumwa moja kwa moja kwenda kwenye akaunti za shule. Urahisi huu wa mtiririko wa fedha unawezekana kwa vile shule za sekondari, tofauti na za msingi, hazihitaji kushughulika na idara nyingi kwenye mkondo wa kupitishia fedha. Hata hivyo, kama ilivyo kwenye elimu ya msingi, fedha za ruzuku kwa wanafunzi na ruzuku ya maendeleo zinachelewa kufika shuleni.

Mathalan, mgawo wa kwanza wa ruzuku kwa wanafunzi mwaka 2007/08, kwa wastani ulipokelewa shuleni mwezi Novemba/Desemba 2007, karibu miezi 5 hadi 6 baada ya kuanza mwaka wa fedha. Huu ni wastani tu, kuna tofauti kubwa ya muda wa kupokea fedha kati ya shule na shule. Baadhi ya shule zilisubiri kwa takriban miezi miwili kabla ya kupata ruzuku kwa wanafunzi; zingine zililazimika kusubiri kwa kati ya siku 257 na 474 kabla ya kupokea ruzuku.

**Jedwali 1: Mwaka wa fedha 2007/08 muda uliopita kabla ya shule kupokea ruzuku kwa wanafunzi-wastani wa idadi ya siku**

| **Eneo ilipo shule** | **Wastani** | **Kiwango cha chini** | **Kiwango cha juu** |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 137 | 100 | 257 |
| Nyingine za mjini | 146 | 72 | 269 |
| Kijijini | 185 | 43 | 474 |
| **Aina ya shule** | **Wastani** | **Kiwango cha chini** | **Kiwango cha juu** |
| za jamii/kata | 165 | 43 | 474 |
| za serikali | 172 | 100 | 269 |
| Jumla kuu | 165 | 43 | 474 |

Hali kama hii inaonekana pia kwenye ruzuku ya maendeleo, ambapo mgawo wa kwanza kwa wastani ulifika shule zilizoko vijijini siku 225 baada ya mwaka kuanza. Wakati tarehe rasmi ya kutoa fedha kutoka hazina ndogo haikuweza kujulikana, inawezekana kabisa kuwa ucheleweshaji mwingine unafanywa na benki. Hii ni pale ambapo matawi ya benki yanachelewa kuhamisha fedha kwenda kwenye akaunti husika licha ya kupokea maagizo ya kufanya hivyo kutoka hazina ndogo. Matokeo ya Ufuatiliaji kwa upande wa elimu ya msingi yanabainisha kwamba, mbali na ucheleweshwaji unaotokana na urasimu uliopo serikalini, baadhi ya matawi ya benki yalicheleweshа kuingiza fedha kwenye akunti za shule hata baada ya kupewa maelekezo ya kufanya hivyo. Pia katika baadhi ya maeneo, fedha zilizoingizwa kwenye akaunti zilikuwa chache kuliko kiasi kilichotajwa kwenye maelekezo toka hazina ndogo kwenda benki.

**Jedwali 2: Muda wa kupokelewa shule mgawo wa kwanza wa ruzuku ya maendeleo-wastani wa idadi ya siku, Mwaka 2007/08**

| **Eneo ilipo shule** | **Wastani** | **Kiwango cha chini** | **Kiwango cha juu** |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 230 | 137 | 290 |
| nyingine za mjini | 191 | 109 | 302 |
| Kijijini | 245 | 29 | 476 |
| **Aina ya shule** | **Wastani** | **Kiwango cha chini** | **Kiwango cha juu** |
| za jamii/kata | 221 | 29 | 476 |
| Za serikali | 302 | 302 | 302 |
| **Jumla kuu** | **225** | **29** | **476** |

Matokeo ya ufuatiliaji yanaonesha kwamba serikali imedhamiria kupeleka rasilimali shuleni kupitia Halmashauri kama sehemu ya sera yake ya ugatuzi wa madaraka. Hata hivyo, kuwepo kwa mikondo mingi ya kupitishia rasilimali kwa ajili ya shule za msingi, na ucheleweshwaji wa fedha unaotokana na fedha kupitishwa Halmashauri , ni viashiria kwamba kupeleka fedha moja kwa moja shuleni bado ni utaratibu mzuri zaidi. Kinachohitajika zaidi ni kuinua  ufanisi kwenye mchakato wa kushughulikia migawo ya fedha kwa kupunguza urasimu serikalini na kuhakikisha kwamba benki zinaingiza fedha kwenye akaunti za shule kwa muda uliopangwa.

### Jambo la 4: Shule za vijijini zina walimu wachache kuliko shule za mjini

Shule za maeneo ya vijijini zina uwiano mkubwa zaidi wa wanafunzi kwa mwalimu kuliko shule za mijini. Hii ina maana kuwa walimu wa vijijini wanahudumia wanafunzi wengi zaidi kuliko wenzao wa mijini. Kwa kuzingatia data za PETS, tukiwahesabu walimu wote wa leseni (walimu walio na cheti cha kidato cha 6 tu) na idadi ya walimu kwenye orodha ya malipo ya mishahara ya walimu walioajiriwa na serikali, mwalimu wa Dar es Salaam na maeneo mengine ya mijini anahudumia kati ya wanafunzi 28 na 29. Wakati huo huo  mwalimu aliyeko  maeneo ya vijijini anahudumia wanafunzi 34. Kwa kuangalia walimu walio kwenye orodha ya serikali ya walipwaji, mwalimu mmoja anahudumia wanafunzi 32 Dar es Salaam, wakati walimu kwenye maeneo mengine ya mijini na vijijini wanahudumia, kwa wastani, wanafunzi 43. Ipo pia tofauti kubwa kati ya shule na shule na kati ya mijini na vijijini kama inavyoonekana katika jedwali 3 hapo chini.

**Jedwali 3: Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu shule za sekondari za mjini na za vijijini**

| Walimu wote (wakiwemo wa leseni) | Wastani | Idadi ya chini | Idadi ya juu |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 29 | 17 | 42 |
| Kwingine mijini | 28 | 6 | 81 |
| Maeneo ya vijijini | 34 | 7 | 62 |
| **Jumla** | **29** | **6** | **81** |
| **Walimu walio kwenye orodha ya serikali ya walipwaji** | **Wastani** | **Idadi ya chini** | **Idadi ya juu** |
| Dar es Salaam | 32 | 17 | 50 |
| Kwingine mijini | 43 | 14 | 119 |
| vijijini | 43 | 8 | 71 |
| **Jumla** | **41** | **8** | **119** |

### Jambo la 5: Shule za Kata zina walimu wachache zaidi kuliko shule za serikali

Shule za kata[1] zinakabiliwa na uhaba mkubwa zaidi wa walimu ikilinganishwa na shule za serikali. Ukiangalia uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi, unaweza kuona kwamba walimu wa shule za kata wana wanafunzi wengi zaidi wa kuhudumia kuliko walimu walio shule za

[1] Shule za jamii/kata kwa kiwango kikubwa zimejengwa na michango ya *wananchi* na msaada kidogo upande wa miundombinu kutoka serikalini. Mara shule ya kata inapofunguliwa, serikali huombwa kupeleka walimu kwenye shule hiyo. Kwa mujibu wa PETS, idadi kubwa ya wakazi wa vijijini inategemea shule za sekondari za kata kwa elimu ya watoto wao, wakati maeneo ya mijini kwa kiwango kikubwa yanahudumiwa na shule za sekondari za serikali.

serikali. Mwalimu wa shule ya kata ambaye yuko kwenye orodha ya serikali ya walipwaji anahudumia wastani wa wanafunzi 43 wakati mwalimu wa shule ya serikali anahudumia wanafunzi 18 tu. Mzigo wa majukumu aliyonayo mwalimu wa shule ya kata ni zaidi ya mara mbili ya mzigo wa kazi wa mwalimu wa shule ya serikali (jedwali 4).

**Jedwali 4: Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu katika shule za jamii/kata na shule za serikali**


| **Walimu wote(wakiwemo wa leseni)** | **Wastani** | **Idadi ya chini** | **Idadi ya juu** |
|---|---|---|---|
| Shule za kata | 29 | 6 | 81 |
| Shule za serikali | 16 | 7 | 25 |
| **jumla** | **29** | **6** | **81** |
| **Walimu walio kwenye orodha ya serikali ya walipwaji** | **Wastani** | **Iddi ya chini** | **Idadi ya juu** |
| Shule za kata | 43 | 14 | 119 |
| Shule za serikali | 18 | 8 | 29 |
| **Jumla** | **41** | **8** | **119** |

Shule za kata zinajitahidi kuondokana na upungufu wa walimu kwa kutumia michango ya shule kuajiri walimu kwa mikataba, na/au kuwalipa posho walimu kutoka shule za sekondari za serikali zilizo jirani kuja kufundisha shule za kata kwa muda. Na kwa vile idadi kubwa ya watu waishio vijijini wana kipato cha chini, hii ina maanisa kuwa wanabeba mzigo mkubwa zaidi wa gharama za ziada za kuajiri walimu kufundisha katika shule zao kuliko wenzao wa maeneo ya mijini wenye uwezo mzuri kiuchumi na ambako walimu wengi wanalipwa na serikali.

## Jambo la 6: Shule za serikali na zile za mijini zina walimu wengi wenye sifa kitaaluma

Walimu wengi zaidi wa shule za kata hawana sifa kitaaluma ukilinganisha na walimu walioko katika shule za serikali. Vivyo hivyo, walimu walio maeneo ya vijijini kwa ujumla wasio na sifa kitaaluma ni wengi zaidi ukilinganisha na wenzao wa mijini. Kama inavyooneshwa na mchoro 3 hapo chini, sehemu kubwa ya walimu wa shule za sekondari za serikali wana shahada za Chuo Kikuu, wakifuatiwa na walimu wenye stashahada (diploma). Ni shule chache sana za serikali huajiri walimu waliohitimu kidato cha VI tu (walimu wa leseni). Kwa upande mwingine, walimu wenye elimu ya kidoto cha sita tu wanachukua karibu asilimia 30 ya walimu wote waliopo shule za sekondari za kata.

**Mchoro 3: Makundi ya walimu kwa sifa zao maeneo ya vijijini/mjini na shule za kata/ za serikali**




## Jambo la 7: Shule za serikali zina rasilimali zaidi kwa ajili ya nyenzo za kufundishia

Kwa kuangalia matumizi kwa ajili ya nyenzo za kujifunzia na uwiano wa gharama za malipo ya walimu kwa mwanafunzi, tofauti kubwa inaonekana kati ya mjini/vijijini, na kati ya shule za serikali na zile za kata, kama inavyooneshwa kwenye jedwali 5 hapo chini. Kwa upande wa vitabu na vifaa vya kufundishia, shule za mijini, hasa shule zilizo jijini Dar es Salaam, zinatumia fedha nyingi zaidi kwa kila mwanafunzi kuliko shule za vijijini. Likija suala la gharama za walimu, shule za vijijini hasa shule za sekondari za kata zinatumia kiasi kikubwa kutokana na rasilimali zao kuajiri walimu wa ziada ili kuziba pengo la upungufu wa walimu. Shule za kata/jumuiya na shule za vijijini zinatumia fedha nyingi kwenye ujenzi ambazo zinatokana na ukweli kwamba, shule nyingi zilifunguliwa kabla ya ujenzi wake kukamilika vizuri.

**Jedwali 5: Muundo wa matumizi ya shule za sekondari ki-shule kiasi kwa kila mwanafunzi**


| Mahari iliko shule | Walimu walio kwenye orodha ya walipwaji | Walimu wasio kwenye orodha ya walipwaji | Vitabu vya kiada /vifaa vya kufundishia | Vifaa vya ofisini | Chakula cha shule | Ujenzi. /ukarabati | samani & marekebisho | Mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 2084 | 1713 | 10227 | 4687 | 1733 | 8587 | 938 | 6304 |
| Miji Mingine | 3501 | 2764 | 7673 | 3077 | 3473 | 15907 | 918 | 2897 |
| Vijijini | 3220 | 6906 | 6754 | 3644 | 16070 | 12254 | 1942 | 6211 |
| **Aiana ya shule** | **Walimu walio kwenye orodha ya walipwaji** | **Walimu wasio kwenye orodha ya walipwaji** | **Vitabu vya kiada /vifaa vya kufundishia** | **Vifaa vya ofisini** | **Chakula cha shule** | **Ujenzi. /ukarabati** | **samani & marekebisho** | **Mengineyo** |
| Jamii/kata | 2947 | 8825 | 7383 | 3755 | 3721 | 13479 | 1558 | 5137 |
| Serikali | 3858 | 2402 | 11850 | 3547 | 59197 | 2904 | 132 | 6698 |
| Jumla | 3036 | 5490 | 7821 | 3735 | 9160 | 12442 | 1418 | 5290 |

## Jambo la 8: Kuna utoro mkubwa wa walimu

Utoro wa walimu ulionekana katika asilimia 56 ya shule zilizofanyiwa ufuatiliaji, na katika baadhi ya shule karibu asilimia 70 ya walimu hawakuwepo kazini wakati data hizi zinakusanywa. Utoro wa walimu ni tatizo kubwa zaidi katika shule za vijijini kuliko shule za mijini, na katika shule za serikali kuliko shule za kata/jamii (Mchoro 4). Idadi kubwa ya walimu ambao hawakuwepo shuleni (asilimia 89 ) walikuwa ni walimu wanaolipwa na serikali kuu. Cha kushangaza, sababu za utoro wa walimu wengi kati ya hawa zilikuwa hazifahamiki kwa utawala wa shule.

Kwa kuwa mishahara ya walimu inachukua sehemu kubwa zaidi kwenye bajeti ya elimu, utoro wa walimu kwenye maeneo yao ya kazi una maana kwamba mabilioni ya fedha yanapotea bure. Bila kuwa na ufuatiliaji makini zaidi, na kuimarishwa kwa mfumo wa ufuatiliaji na uwajibikaji, fedha mpya zinazowekezwa kwenye elimu zinaweza kushindwa kuleta matokeo bora katika ujenzi wa jamii yenye ujuzi zaidi.

**Mchoro 4: Asilimia ya walimu watoro kama sehemu ya walimu wote shuleni-data za uchunguzi**




## Jambo la 9: Shule za kata na shule za maeneo ya vijijiji hufanya vibaya zaidi kwenye mitihani


PETS inatumia viwango vya ufaulu wa mitihani kama kigezo cha kutathmini ubora wa elimu na mafunzo shuleni. Inaonesha kwamba shule za serikali kwa ujumla zina ufaulu mzuri zaidi kwenye mtihani wa kumaliza kidato cha nne (*Certificate of Secondary Education Examination*) kuliko shule za kata. Vivyo hivyo, shule za mijini zina ufaulu mzuri zaidi kuliko shule za vijijini. Hali hii inaonekana kwenye mitihani yote, ya kidato cha II na ya kidato cha IV (Mchoro 5).

Badala ya idadi ya walimu, au uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi, ufaulu huu unahusiana zaidi na sifa walizo nazo walimu. Shule zenye walimu wenye sifa za juu kitaaluma zina ufaulu wa juu kuliko shule zenye walimu wenye sifa za chini kitaaluma, bila kujali uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi uliopo shuleni. Pia ilibainika kuwa

shule zenye walimu wengi wenye sifa za juu kitaaluma zinapata rasilimali zaidi na zina matumizi ya juu yanayohusiana na malipo ya ujira. Hata hivyo, ni vigumu kuamua iwapo kigezo hiki (sifa za walimu) ndio chanzo cha ufaulu. Hivyo ni vema viangaliwe vigezo vingine pia kama vile uwezo wa kiuchumi wa wanafunzi au kiwango cha elimu cha wazazi wao.

Licha ya tahadhari hii, data zinaibua maswali kuhusu vitendo vya kuchukua walimu wa mikataba wenye sifa zisizotosheleza kuhudumia shule za kata na athari zake kwenye ufanisi wa elimu.

**Mchoro 5: Kiwango cha ufaulu kidato cha II na cha IV –data za uchunguzi 2008**




## Jambo la 10: Menejimenti ya taarifa ni dhaifu, kutofautiana kwa data ni kitu cha kawaida mno

Mfumo makini wa uwajibikaji unahitaji kwamba taarifa za fedha na data nyingine za shule zikusanywe, zichambuliwe, zihifadhiwe na ziripotiwe kwa namna ambayo inatoa wepesi wa kufuatilia rasilimali hadi ngazi za chini kabisa fedha zinakotumika, yaani shule. Uhakiki wa usahihi wa taarifa zinazoandaliwa katika ngazi mbalimbali unaweza pia kufanyika ili kuhakikisha kuwa taarifa zinazotolewa ni sahihi na za kuaminika kwa matumizi ya ki-sera.

Hata hivyo, PETS ilibaini matatizo kadhaa kwenye eneo hili. Taarifa za orodha ya walipwaji kwenye ofisi ya menejimenti ya utumishi wa umma (Ofisi ya Rais-Menejimenti ya utumishi wa umma (PO-PSM) haziweki mazingira yanayowezesha kufuatilia rasilimali za ujira/mishahara (*Personnel Emoluments*) mpaka ngazi ya shule iliyolengwa kunufaika. Ngazi ya chini ambayo inaweza kufikiwa ni 'kituo cha malipo' ambacho huwa ni shule mojawapo wanapolipiwa walimu toka shule nyingine nyingi. Hadi wakati wa uchunguzi wa PETS sio hazina ndogo za mikoa wala shule zilizokuwa na data za malipo ya ujira au mishahara (PE) kwa kila shule.

Zaidi ya hilo, mfumo wa kuhifadhi data (*Education Managemement Information System) (EMIS)*) wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ulikuwa na taarifa zinazokinzana kuhusu idadi ya shule katika mwaka wa shule ikilinganishwa na data kwenye faili la shule zilizoandikishwa ambayo pia inamilikiwa na wizara hiyohiyo.

Kutokuwepo kwa alama maalumu za utambulisho wa shule, mahali shule zilipo pamoja na umiliki wake, kunamaanisha kwamba shule ileile moja inaweza kuonekana kwenye makundi ya wamiliki tofauti kwenye hifadhi za data tofauti. Kutokana na makosa yanayojitokeza katika kuandika majina na wakati wa kuziweka kwenye makundi, baadhi ya shule binafsi ziliwekwa kwenye kundi la shule za serikali na iliripotiwa kuwa zilipangiwa ruzuku ambayo hazikustahili kupata. Zaidi ya hapo, hifadhidata ya EMIS, fomu za TSS na data zilizopo katika ngazi ya shule zinatoa taarifa zisizolingana.

Mapungufu haya yanaibua maswali ya kiwango cha uaminika wa taarifa zinazoandaliwa kutoka kwenye mfumo mzima wa menejimenti ya taarifa za elimu, na iwapo zinafaa kutumiwa kufanya mipango na kuandaa sera. Kwa madhumuni ya usimamizi wa uwajibikaji, ni muhimu kwamba ubora na kiwango cha uchambuzi wa taarifa zinazohusu nyanja zote za mfumo wa elimu viboreshwe, na taarifa ziwekwe wazi kwa wote.

## 3. Hitimisho

Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma unaonesha kuwa fedha kwa ajili ya elimu ya sekondari zimepungua kwa kiwango kikubwa katika miaka ya hivi karibuni. Hali hii inaibua maswali iwapo rasilimali zinazotengwa zinatosha kusaidia kufikiwa kwa lengo la kutoa elimu bora na kuleta usawa kwa wote.

Zaidi ya hayo, fedha zinachelewa kufika shuleni, na mbali na fedha kwa ajili ya malipo ya mishahara na masurufu (ambazo hufika kwa kiwango kamili), ni mara chache sana rasilimali nyingine hutolewa zikiwa kamili/sawa na maidhinisho. Hii inadhoofisha utekelezaji wa bajeti.

Ufuatiliaji pia umeonesha kuwa shule za kata na shule zilizo maeneo ya vijijini zinapata rasilimali kidogo; kwamba shule za vijijini na shule za kata zina walimu wachache zaidi wenye sifa na kwamba kiwango cha utoro wa walimu ni kikubwa zaidi maeneo ya vijijini kuliko maeneo mengine. Matokeo yake ni kuwa shule za vijijini na za kata zinafanya vibaya kwenye mitihani ya kidato cha nne.

Taarifa zinazoandaliwa katika ngazi mbali mbali kwenye mfumo wa elimu pia hazifanani, na hivyo kuibua maswali ni kwa kiwango gani taarifa hizi zinaweza kuaminika au ni sahihi kuweza kutumiwa kwa madhumuni ya sera na mipango.

Nini kifanyike kurekebisha matatizo haya? Tunapendekeza hatua nne zifuatazo:

1. Tenga fedha zaidi kwa kila mwanafunzi wa elimu ya sekondari. Rasilimali zinapaswa kuongezwa ili kukidhi mahitaji na malengo kusudiwa. Ongeza rasilimali kwa ajili ya vifaa/nyenzo za kujifunzia na kufundishia kwa shule za vijijini na za kata.

2. Ongeza ufanisi katika mchakato wa kupeleka fedha shuleni kwa kuondoa urasimu usio wa lazima kwenye mkondo wa upelekaji fedha. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuhakikisha kuwa serikali inashughulikia utumaji wa fedha kwa wakati na inazilazimisha benki kuhamisha fedha mara moja kwenda kwenye akaunti za shule.

3. Peleka walimu zaidi na wenye sifa shule za vijijini na shule za kata. Shughulikia sababu zinazowavunja moyo walimu wenye sifa kufanya kazi maeneo ya vijijini na shule za kata. Hili linaweza kufanyika kwa kuweka motisha ya kuwavutia walimu wengi kwenda maeneo ya vijijini, mathalan, kwa kuwapa walimu wa vijijini mishahara mikubwa na marupurupu mengine kuliko walimu wa mijini.

4. Boresha mfumo wa uandaaji, utunzaji na uwasilishaji wa taarifa kwenye sekta kwa kuweka utaratibu wa kusahihisha kasoro katika data kuhusu nyenzo mbalimbali (upangaji walimu, uandikishaji wa shule, n.k). Sera nzuri zinahitaji menejimenti ya taarifa inayoaminika.

Haya yanaweza kufanyika; kinachohitajika ni nia na jitihada madhubuti ya kuyatekeleza!

## Rejea

URT (2010), "*Public Expenditure Tracking Survey of primary and secondary Education, Final report*" , Februari 2010, Dar es Salaam, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.